*Nordic Journal of African Studies 15(2): 143–153 (2006)*

# Matatizo Yanayowakumba Waandishi wa Vitabu vya Kiswahili Nchini Kenya*

JOHN M. KOBIA†
*Kenyatta University, Kenya*

## ABSTRACT

This article addresses the problems facing Kiswahili authors in Kenya. It focuses on socio-economic, technological, attitudinal and language policy related challenges in relation to Kiswahili language and literature in the 21st century. The article attempts to offer suggestions on the way forward as far as writing of Kiswahili books in the Kenyan education system is concerned.

*Keywords: Uandishi, mfumo wa elimu, matatizo, uchapishaji, vitabu, Kenya*

## 1. UTANGULIZI

Ustawi wa sekta ya elimu umekuwa dhamira ya muda mrefu ya serikali ya Kenya tangu kujinyakulia uhuru. Elimu huchukuliwa na washika dau kama haki na mahitaji ya kimsingi pamoja na faida zinazotokana nayo. Huku tukichunguza nafasi ya Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Kenya, ni vyema tukumbuke kuwa mfumo wa elimu wa nchi yoyote inayotegemea lugha ya kigeni hasa lugha ya waliokuwa watawala wao wa kikoloni huendeleza maadili ya kigeni na utegemeo (Mbaabu 1996).

Ingawa kwa sababu ya utandawazi, lugha huathiriana duniani kote, lugha za kigeni katika mfumo wa elimu hunuia kuendeleza maadili na utamaduni wa kigeni ambayo mengi yayo hayaambatani wala kulingana na matarajio na mahitaji ya kimaendeleo ya nchi kama ya Kenya. Kwa hivyo, ni muhimu sisi kama wataalamu, watafiti na wasomi wa lugha ya Kiswahili tujaribu kuipa nafasi inayostahiki lugha hii katika mfumo wetu wa elimu. Njia mojawapo ya kufanikisha lengo hili bila shaka ni kuwepo kwa vitabu vya Kiswahili vinavyotumiwa katika mfumo wa elimu.

Uandishi wa vitabu huchangia pakubwa katika kufanikisha malengo ya elimu katika nchi yoyote iwayo. Lakini uandishi na waandishi hukabiliwa na changamoto kadhaa katika kutimiza wajibu huu. Ingawa waandishi kwa ujumla

---

* Makala hii iliwasilishwa katika KONGAMANO LA CHAKITA – KENYA kwenye mada kuu: KISWAHILI KATIKA MIFUMO YA ELIMU Fort Jesus, Mombasa, Kenya, Septemba 30, 2005.

† Mwandishi ni mwanafunzi wa shahada ya uzamifu (P.hD) katika Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. Nyanja zake za utafiti ni pamoja na masuala ya uana, fasihi simulizi, isimujamii, mawasiliano na uchapishaji.

hukumbwa na matatizo yanayozuka kila siku katika taaluma yao, waandishi wa vitabu vya Kiswahili hukumbana na matatizo chungu nzima.

Makala hii inadahili na kudadavua matatizo ya kisera, kiuchumi, kimielekeo, kiitikadi, kijamii na kielimu yanayowakumba waandishi wa vitabu vya Kiswahili katika mifumo ya elimu nchini Kenya. Aidha, makala hii inapendekeza hatua zinazoweza kuchukuliwa kuimarisha hali ya uandishi wa vitabu vya Kiswahili nchini Kenya na mustakabali wake.

Kuna aina mbalimbali ya vitabu vya Kiswahili. Kuna vitabu vya kiada, vitabu vya ziada na vitabu vya marejeo. Makala hii itazingatia zaidi vitabu vya kiada na vile vya ziada hasa vinavyotumiwa katika shule za msingi na za upili nchini Kenya.

## 2. LUGHA YA KISWAHILI KATIKA MFUMO WA ELIMU NCHINI KENYA

Masuala ya historia ya sera ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya yako nje ya mipaka ya makala hii. Hata hivyo, tutadurusu japo kwa ufupi, hali ya lugha ya Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Kenya.

Kwa sasa nchini Kenya hakuna sera madhubuti ya lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, masuala yanayoweza kuitwa sera ya lugha ya Kiswahili yanaweza kupatikana katika tume za elimu kadhaa zilizoundwa zinazoathiri lugha ya Kiswahili hasa katika mfumo wa elimu. Lakini Tume ya Mackay ya 1981 ndiyo iliyokuwa na taathira kubwa zaidi kwa lugha ya Kiswahili. Tume hii ilipendekeza lugha ya Kiswahili kufundishwa na kutahiniwa kama somo katika mfumo wa elimu kuanzia shule za upili hadi katika vyuo vikuu. Mwaka wa 1985, ulijenga msingi thabiti wa lugha ya Kiswahili, kwani kwa mara ya kwanza lugha ya Kiswahili ilitahiniwa katika mtihani wa K.C.P.E. katika mfumo wa elimu wa 8-4-4 (Mbaabu, 1996: 131).

Mfumo wa elimu huathiri uandishi wa vitabu. Kubadilika kwa mfumo wa elimu nchini Kenya kutoka mfumo wa 7-4-2-3 hadi ule wa 8-4-4, kulisababisha kuathirika kwa mitaala. Kubadilika kwa mitaala bila shaka hupelekea uandishi upya wa vitabu ili viambatane na matakwa ya silabasi mpya.

Hadi sasa lugha ya Kiswahili ni somo la lazima katika shule za msingi na sekondari nchini Kenya. Hali hii imesababisha haja ya kuandika vitabu vya Kiswahili vya kiada na vya ziada ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi. Lakini je, vitabu vya kiada ni vipi? Na vile vya ziada ni vipi? Je, waandishi wa vitabu hivi hukumbana na matatizo yapi katika jitihada zao za uandishi? Je, matatuzi ni yapi? Maswali haya ya kimsingi, kwa hakika ndiyo kiini cha makala hii.

Kwa mujibu wa Mbunda (1983: 1) vitabu vya kiada ni vile ambavyo ndani yake mna maarifa na stadi kufuatana na malengo ya elimu. Kwa kawaida katika lugha ya Kiswahili stadi hizi huwa ni kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika pamoja na maarifa yanayohusu sarufi na msamiati. Stadi na maarifa haya hupangwa kwa utaratibu maalumu kutoka kiwango cha chini hadi cha juu

kufuatana na mtaala. Vitabu vya kiada hutimiza malengo ya silabasi katika kiwango fulani katika somo husika. Baadhi ya mifano ya vitabu vya kiada vya lugha ya Kiswahili katika shule za upili ni *Kiswahili Mufti*, *Kiswahili kwa Darasa*, *Masomo ya Msingi*, *Kiswahili Sanifu*, *Kina cha Kiswahili*, *Kiswahili Teule*, *Msingi wa Kiswahili* miongoni mwa vingine. Katika shule za upili vitabu vya kiada vya Kiswahili ni kama vile *Kiswahili kwa Kidato*, *Chemchemi za Kiswahili*, *Kiswahili Fasaha*, *Uhondo wa Kiswahili*, *Johari ya Kiswahili* miongoni mwa vingine. Ufundishaji wa lugha ya Kiswahili hutegemea kwa kiwango kikubwa vitabu vya kiada hivyo basi waandishi wa vitabu hivi sharti wafuate silabasi katika uandishi wao.

Vitabu vya ziada kwa upande mwingine ni vitabu vya nyongeza, ni vitabu zaidi ya vile vya lazima katika kutimiza matakwa ya silabasi (Mbunda, 1983: 1). Kwa kawaida vitabu vya ziada hujengwa juu ya misingi ya vitabu vya kiada. Vitabu vya ziada husaidia kupanua stadi na maarifa yanayopatikana katika silabasi. Vitabu vya ziada katika shule za msingi ni kama vile hadithi za watoto, vitabu vya mazoezi na marudio, na vinginevyo. Vitabu vya marejeo ni kama vile kamusi mbalimbali.

## 3. Matatizo Yanayowakabili Waandishi wa Vitabu vya Kiswahili

Baadhi ya mashirika ya uchapishaji hayako tayari kuchapisha vitabu vya waandishi chipukizi. Jambo hili huwavunja nyoyo waandishi wa Kiswahili ambao wangependa kujiendeleza kitaaluma kupitia uandishi wa vitabu vya riwaya, tamthilia, ushairi, hadithi fupi na fasihi ya watoto. Suala hili ni la kusikitisha kwani imedaiwa kuwa baadhi ya mashirika ya uchapishaji huchapisha majina ya waandishi na wala sio uzito na ufaafu wa kazi yenyewe. Hili hutokea hasa pale mwandishi ametunga kwa mfano riwaya na kisha ikateuliwa kutumiwa kama kitabu cha fasihi kutahiniwa katika shule za upili. Mwandishi huyo akiandika kazi yoyote nyingine ya kisanaa, ingawa huenda si ya kiwango cha juu kama ile ya kwanza, kuna uwezekano wa mchapishaji, kuangukia mtego wa kuichapisha kazi ile na kupuuza zile za waandishi chipukizi. Hoja hii inashadidiwa na kilio cha mwandishi wa vitabu vya Kiswahili, Njama (2005) kuwa:

> Tatizo la kwanza linaanzia kwa wachapishaji. Kama hujajulikana kwenye uwanja wa uandishi, kazi yako haiangaliwi kwa undani sana na mhariri katika shirika la uchapishaji. Mswaada huchukua muda mwingi kutathiminiwa. (Mahojiano kwa njia ya baruapepe)

Ukosefu wa soko ni tatizo lingine linalowakabili waandishi wa vitabu vya Kiswahili. Iwapo mwandishi atachapisha kazi yake na kazi hiyo haina nafasi katika mfumo wa elimu hasa shule za msingi na upili, huenda asipate mauzo mengi. Hili ni kwa sababu mfumo wa elimu nchini Kenya umeibua utamaduni

wa kusoma kwa minajili ya kupita mitihani huku dhima nyingine za kusoma zikiwekwa pembeni. Ni kweli kwamba kazi ya uandishi huhitaji kujitolea na kujinyima mengi. Na iwapo juhudi za waandishi hazizai matunda kwa njia ya kulipwa mrabaha, huvunjwa nyoyo.

Chachage (1993: 25) ameshadidia tatizo la kutegemea soko la shule kuwa:

> Ni kweli kwamba nchi yetu ina njaa ya vitabu (hasa vya Kiswahili). Hili linakubalika na watu wengi hata wale wanaolalamika kuwa hakuna tabia (utamaduni) wa usomaji. Mashule na vyuo ndiyo masoko yategemewayo na mashirika mengi ya uchapishaji na maduka ya vitabu. Tangu tupate uhuru, mashirika ya uchapishaji na maduka ya vitabu yameshughulika zaidi na vitabu vya mashule na masomo kwa ujumla katika ngazi mbalimbali kama njia pekee na rahisi kuishi.

Uandishi wa vitabu vya Kiswahili mara nyingi huamuliwa na mahitaji ya shule. Wakati mwingine mashirika ya uchapishaji husita kuchapisha kazi ambazo haziwezi kuingizwa katika mfumo wa elimu kama kitabu cha kiada au ziada. Hii ni kwa sababu, soko kubwa la wachapishaji wengi ni shule.

Katika mfumo wa elimu nchini Kenya, vitabu ambavyo hununuliwa ili kutumiwa shuleni hasa katika shule za msingi ni vile vilivyoidhinishwa na kupitishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolojia kupitia Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE). Ingawa kitabu cha kiada au za ziada kinaweza kuwa mwafaka, mradi hakipo katika kijitabu kinachotolewa na Wizara kiitwacho “Orange Book”, hakiwezi kununuliwa na shule za umma huku ikizingatiwa shule hizi ndizo zenye idadi kubwa ya wanafunzi.

Miswaada ya Kiswahili haitiliwi maanani sana na wachapishaji kwani wanaona kama haina soko. Ni kweli kuwa kila mchapishaji ni mfanyibiashara na kawaida ya kila mfanyibiashara sharti awe na dhamira ya kupata faida kwa kutumia raslimali chache iwezekanavyo. Sekta ya uchapishaji ikiwa ni sekta ya uwezekaji, inafanya kuwa vigumu kwa mchapishaji kuwekeza katika miradi anayodhani haitamletea faida. Wachapishaji wengi nchini Kenya hufikiri kwamba soko la Kiswahili si pana kama lile la Kiingereza. Hali hii inaeleza kuwepo kwa vitabu vingi vya fasihi ya watoto kwa lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili.

Kuna waandishi wengi wa vitabu vya Kiingereza nchini Kenya kuliko wale wa Kiswahili. Kwa mfano, orodha ya vitabu vya ziada vya Kiingereza vilivyoidhinishwa kutumiwa katika shule za msingi katika darasa la kwanza mwaka wa 2005 ni 101 ilhali vya Kiswahili ni 19 pekee. Vitabu vya ziada vya Kiingereza vilivyopitishwa kutumiwa katika shule za msingi kutoka darasa la kwanza hadi la nane mwaka wa 2005 ni 659 huku vya Kiswahili vikiwa ni 27 pekee (MoE, 2005).

Uteuzi wa vitabu vitakavyotumiwa vya fasihi ya Kiswahili katika shule za upili unaofanywa na Taasisi ya Elimu ya Kenya, bado umekumbwa na lawama kutoka kwa washika dau kadhaa, wakiwemo waandishi. Imedaiwa kuwa wanaoteua vitabu hivyo huchagua majina ya waandishi na wala sio yaliyomo kwenye vitabu hivyo hata kama maudhui yaliyomo katika vitabu hivyo

yamepitwa na wakati (Njama, 2005). Aidha, kasumba kuwa ni waandishi kutoka Tanzania ambao wanaweza kuandika vitabu bora vya Kiswahili hutinga juhudi za waandishi kutoka Kenya, kujiimarisha kitaalamu hasa vitabu vyao vinapokataliwa kutahiniwa katika mfumo wa elimu nchini Kenya.

Vitabu vingi vya kiada na ziada nchini Kenya kwa sasa vilivyokusudiwa kutumiwa shuleni huteuliwa na Taasisi ya Elimu ya Kenya (K.I.E.). Vitabu vilivyoteuliwa huwekwa kwenye kijitabu kinachoandaliwa na Wizara ya Elimu, hawaoni haja ya kukitangaza sana kwani huamini kuwa kitauzwa tu mradi kiko kwenye "Orange Book". Hata hivyo mashirika ambayo vitabu vyao havijateuliwa hufanya uzambazaji, uuzaji wa nguvu na huvitangaza vitabu vyao magazetini, redioni na runingani.

Biashara kubwa ya vitabu kokote duniani iko katika vitabu vya kiada na ziada vinavyotumiwa shuleni. Baadhi ya waandishi huandika miswaada ambayo haina hadhira maalumu. Wale waandishi ambao huandika vitabu ambavyo hulenga hadhira pana ya wanafunzi wa shule za msingi na upili hufaidika kimauzo.

Mwandishi wa vitabu vya Kiswahili pia anaweza kuwa na matatizo ya kimaudhui na kifani katika uandishi wake. Kwa kawaida mwandishi huwa na wazo ambalo anataka kuwasilisha kwa hadhira yake kupitia maandishi. Baadhi ya waandishi, ijapokuwa wana wazo, hawajui waanze vipi, walikuze vipi na kuliendeleza vipi.

Tatizo la maudhui yapi yanayopaswa kuandikwa mara nyingi huwakumba waandishi wa Kiswahili. Kilicho muhimu kwa mwandishi ni kutambua kiwango cha umuhimu na uzito wa maudhui kutoka jamii yetu ya kisiasa. Ingawa maudhui ya uchawi, mapenzi, uhalifu yalishmiri sana katika kazi za uandishi wa Kiswahili miaka ya nyuma, bado kuna baadhi ya waandishi ambao hung'ang'ania kuandikia maudhui hayo.

Mfumo wa elimu nchini Kenya, hasa katika shule za msingi na za upili haujatilia mkazo somo la utunzi wa kisanaa kwa muda mrefu. Ingawa silabasi mpya inapendekeza utunzi wa kazi za kisanaa ufundishwe jambo hili halitiliwi maanani kwa sababu mada hii haitahiniwi katika mtihani wa kidato cha nne.

Nchini Kenya hakujawa na chuo cha uandishi, ambacho kingekuwa na jukumu la kutoa mafunzo kwa waandishi. Chuo kama hiki kinaweza kuwa chini ya Wizara ya Elimu au ile ya Utamaduni. Ingawa uandishi ni kipawa, kwa kweli kipawa huitaji kukuzwa na kupaliliwa na njia mojawapo ni kuwa na mafunzo ya kitaaluma kuhusu uandishi.

Uandishi ni taaluma inayohitaji muda. Wengi wa waandishi wa Kiswahili ni walimu wanaofundisha katika ngazi mbalimbali katika mfumo wa elimu. Mara nyingi, walimu huwa na kazi nyingi kama vile kufundisha, kusahihisha, kusimamia kazi za wanafunzi miongoni mwa nyingine. Baadhi ya wahadhiri huwa na kazi nyingi, hivi kwamba wengine wao wanafundisha hata katika vyuo vikuu vitatu kwa wiki moja mbali na shughuli za kinyumbani. Muda kwao huwa haba na taaluma ya uandishi huhitaji muda mwingi.

Katika uandishi wa vitabu suala la utafiti ni muhimu na la lazima. Baadhi ya waandishi wa Kiswahili hawajamakinika katika mbinu za utafiti. Isitoshe,

ukosefu wa marejeo muhimu ni tatizo kubwa kwa waandishi wa Kiswahili. Baadhi ya dhana za kimsingi za kiisimu na kifasihi zinazofundishwa katika mfumo wa elimu, zinahitaji kutafitiwa kwa kina. Aidha, baadhi ya marejeo hayapatikani kwa urahisi na yakipatikana huwa ghali mno kwa mwandishi anayeanza kazi hii ya uandishi. Na ikumbukwe kuwa baadhi ya waandishi wa vitabu vya Kiswahili ni walimu wa shule za msingi na sekondari.

Ukosefu wa vifaa vya kisasa vya uandishi kama vile kompyuta. Vifaa hivi kama vile tarakilishi ni ghali mno ingawa ni muhimu sana katika taaluma ya uandishi. Wachapishaji wengi hawakubali miswaada ambayo haijapigwa chapa.

Waandishi wengi hasa wa vitabu vya sanaa hulazimisha maudhui. Kuna baadhi ya waandishi wanaotaka kuandika kila utanzu yaani thamthilia, riwaya, ushairi, hadithi fupi, vitabu vya watoto na vinginevyo jambo ambao haliwezekani kwa waandishi chipukizi.

Shughuli ya uandishi huhitaji muda mwingi ambao mara nyingi waandishi hawapati kwani wengi wao ni walimu shuleni, au wahadhiri vyuoni au katika shughuli nyinginezo. Hivyo basi wakati wanapohitajika kujumuika pamoja ili waandike vitabu huwa ni vigumu kuwapata wote wakati mmoja hasa pale ambapo vitabu ya kiada huandikwa na kikundi au kijopo.

Mwandishi wa Kiswahili hukumbwa na tatizo hasa anapotaka kuandika na kuchapisha vitabu vingi – kwa mfano kama kumi hivi kwa mwaka – hali ambayo huenda ikaathiri ubora wa vitabu vya Kiswahili. Kinachohitajika ni mwandishi kuandika kazi inayoweza kuhimili mawimbi ya wakati. Tatizo la kuwa na lengo la kuandika vitabu vingi kwa mwaka ni kuwa huenda mwandishi asiweze kupata muda wa kuvishughulikia ipasavyo ikizingatiwa kuwa kazi ya uandishi si kama kazi ya ukulima inayohitaji nguvu tu. Kazi ya uandishi hasa wa vitabu vya Kiswahili inahitaji utafiti wa kina, kujitolea, kujinyima, nguvu za mwili na akili na mazingira tulivu.

Mara nyingi waandishi hawapati ushauri ufaao kuhusu taaluma ya uandishi na masuala yanahohusiana na uchapishaji. Akitoa mfano jinsi kazi yake ilivyokawia kuchapishwa kwa sababu ya kukosa ushauri, Mung’ong’o (1993: 49) anatusimulia:

> …Kazi yangu ya awali kabisa ilikuwa ***Mirathi ya Hatari***. Kazi hii ilianza kuandikwa mapema mwaka wa 1966 nilipokuwa katika kidato cha pili katika Shule ya Sekondari ya Kibana. Lakini kwa sababu ya mzigo wa masomo na kwamba wakati ule sikuwa na mtu wa kunishauri katika masuala hayo ya utunzi sikuweza kuikamilisha kazi hiyo hadi mwaka 1969 …Muswada haukuweza kutoka kama kitabu hadi mwaka wa 1979.

Baadhi ya wachapishaji huwatapeli waandishi, hivi kwamba hawalipi mrabaha kwa waandishi ipasavyo. Wengi wa waandishi wamedai kuwa asilimia 10 wanayolipwa kama mrabaha ni kiwango cha chini mno. Na ni kweli asemavyo Robert (1966: 82) kwamba ‘Mwandishi si mtu wa ajabu awezaye kuishi kwa kula hewa na kunywa ukungu. Ni mtu wa desturi ambaye, kama watu wengine wa desturi hafarijiwi na hasara’. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa shughuli ya

uchapishaji ni shughuli ngumu yenye gharama kubwa kutoka kupokelewa kwa mswaada hadi kitabu kinapomfikia msomaji.

Ili kuelewa barabara matatizo yanayowakumba waandishi, tusome dondoo lifuatalo:

> Popote pale duniani mwandishi wa kitabu anapoketi chini kuandika anategemea vitu vitatu. Kwanza, kitabu chake kitoke vizuri na haraka iwezekanavyo; pili, kisomwe na watu wengi iwezekanavyo; na tatu, apate chochote kutokana na jasho lake. Hivi vikikosekana lazima mwandishi yeyote yule alalamike. (Mallya, 1993: 24).

Kutokana na nukuu hili matatizo yanayowakumba waandishi yanaweza kuelewa kama ni ya kibinafsi, udhaifu wa wachapishaji na kufujwa na baadhi ya wachapishaji. Jambo hili limewapelekea baadhi ya waandishi kuanzisha kampuni zao za uchapishaji, ambazo nyingi huchapisha kazi za mwandishi huyo mmoja. Ingawa hii ni hatua muhimu ya kukabiliana na baadhi ya matatizo yanawakumba waandishi, mara nyingi kampuni kama hizo hukumbwa na matatizo ya uuzaji na usambazaji wa vitabu hadi kwa wasomaji. Hivyo basi kitabu cha mwandishi kinaweza kutoka wakati ufaao lakini kikakosa kusomwa na kusambazwa kwa watu wengi iwezekanavyo. Kutokana na kutowafikia wasomaji wengi bila shaka, mwandishi hupata mapato machache mno kifedha na hili humvunja moyo sana.

Aidha, waandishi hulalamika kuwa hawapati malipo ya mrabaha na kwa wakati uliokubalika. Isitoshe, baadhi ya wachapishaji hawatoi taarifa muhimu kuhusu kitabu cha mwandishi. Taarifa hii ni muhimu kwani sharti kiwe na maelezo kuhusu kitabu kilitoka lini, idadi ya nakala zilizochapwa pamoja na mauzo ya kipindi fulani, mara nyingi kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Tatizo lingine ni lile linalohusishwa na muda ambao muswada huchukua ili utathminiwe na uamuzi kufikiwa. Waandishi wengi hulalamika kuwa muda mrefu hutumika katika kupokelewa kwa muswada hadi kutathminiwa na ripoti kutolewa. Na ni kweli mwandishi huweza kungojea hadi mwaka mmoja au zaidi kabla ya kupokea ripoti ya mchapishaji. Lakini mara nyingi wachapishaji sio wa wa kulaumiwa katika jambo hili. Kwa kawaida wachapishaji huwapa wasomaji wa mswaada kusoma na kutathmini mswada hasa ukiwa na kitaalamu. Wasomaji hawa huchukua muda mrefu kusoma na kutoa tathmini ya mswada. Udhaifu mkubwa wa wasomaji ni kuwa wengi ni wenye kazi nyingi hasa za kufundisha katika vyuo vikuu, kufanya utafiti, kuhudhuria kongamano, kuandika miswada, lakini linalomkatisha tamaa zaidi sio muda mrefu ambao ripoti huchukua kumfikia. La mno ni kuwa ripoti mara nyingi huwa na marekebisho mengi au hukataa muswada mara moja. Mallya (1993: 215) anasema:

> Hakuna kinachoudhi mwandishi kama kurudia tena kazi ambayo alifikiri alikwisha kuimaliza mwaka mmoja uliopita. Kinachokatisha tamaa zaidi ni kule kukataliwa kwa mswada na hivyo nguvu za mtu kupotea bure.

Lakini ningependa kutoa maoni yangu kuwa ni afadhali ripoti ichukue muda mrefu lakini iwe kamilifu na inayotosheleza. Mara nyingi wachapishaji huwapa wasomaji wa miswada wawili kusoma na kutathmini mswada mmoja. Wakati mwingi jina la mwandishi wa mswada huondolewa kwenye mswada ili kuepuka uwezekano a upendeleo.

## 4. MAPENDEKEZO

Nia ya makala hii sio kuwavunja moyo waandishi wa vitabu vya Kiswahili au wanaonuia kuingia katika taaluma ya uandishi, bali huangaza tu hali halisi ilivyo nchini Kenya kwa sasa. Hapa nitajaribu kutoa mapendekezo ambayo ninaamini yakizingatiwa kwa dhati yanaweza kutatua kwa kiasi fulani matatizo yanayowakumba waandishi wa vitabu vya Kiswahili.

Jambo la kwanza ni kuhusu waandishi wenyewe. Kwa sababu kazi ya uandishi inahitaji kujitolea sharti waandishi wajitahidi kufanya utafiti wa kazi wanazoandikia. Inawabidi wajiulize maswali kadha yakiwemo: Wanaandikia nani? Aidha, wawe na marejeo yanayochapishwa kila wakati. Mwandishi bora ni yule anayekwenda na wakati. Mwandishi ajibidiishe kununua tarakilishi kwani hiki ni chombo muhimu katika uandishi. Mwandishi asiyekuwa na tarakilishi siku hizi ni kama mkulima anayeenda shambani bila jembe.

Serikali inaweza kushirikiana na vyama vya kitaaluma na kuanzisha chuo cha mafunzo kuhusu taaluma ya uandishi. Hii itakuwa hatua muhimu sana katika kutoa mafunzo kwa waandishi wa vitabu vya Kiswahili. Hii ni kwa sababu mitaala ya vyuo vikuu haitoi mafunzo kamili kuhusu nadharia na mbinu za uandishi wa vitabu. Chuo kama hicho kinaweza kuwa chini ya Wizara ya Elimu au Wizara ya Utamaduni.

Isitoshe, panahitajika kuandaliwa semina mahsusi kuhusu masuala ya uandishi. Hili linaweza kufanikishwa na Chama cha Waandishi cha Kenya. Semina zinaweza kuwakutanisha waandishi wa tajriba na tabaka mbalimbali na kuweza kubadilishana maoni kuhusu masuala yanayowahusu hususan ya uandishi.

Uhusiano baina ya mwandishi na mchapishaji hauna budi kuimarishwa kwa manufaa ya wote. Kila mmoja anamtegemea mwingine. Hakuna anayeweza kudai kuwa anaweza kuwepo bila ya mwingine. Ushirikiano na kuaminiana ni masuala ya kimsingi lakini yenye umuhimu mkubwa sana kati ya mwandishi na mchapishaji.

Waandishi na wachapishaji sharti waaminiane. Ni kweli kuwa mchapishaji kamwe hawezi kuwepo bila mwandishi. Naye mwandishi hawezi kuwepo bila mchapishaji. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na waandishi ambao kwa sababu moja au nyingine wameanzisha kampuni zao za uchapishaji na kutoa vitabu vyao walivyoandika wenyewe. Hatari iliyopo hapo ni kuhatarisha ubora na utaalamu wa vitabu, kwa sababu si lazima mwandishi mzuri awe ana tajriba pana ya uchapishaji. Hii ni kwa sababu, kama asemavyo

Mallya (1993: 225) "… kuchapisha ni zaidi ya kuandika na kuchapa; ni pamoja na kuhariri, kusambaza na kuratibu shughuli zote hizi."

Kwa hakika gharama kubwa katika sekta ya uchapishaji ni ya mchapishaji si mwandishi. Tazama mahesabu haya:

Mahesabu ya Gharama ya Uchapishaji

1. Uchapaji (kuruwaza, kuchapa na kujalidi) – 30%
2. Kipunguzo (maduka – 20% – Wakala 10%) = 30%
3. Gharama za mchapishaji (uzalishaji, uuzaji, utangazaji, uhasibu, utawala) 20%
4. Mrabaha 10%
5. Faida (kabla ya kodi) 10%

100.00

Kwa kuchunguza maelezo hayo hapo juu itabainika kuwa wachapishaji si kupe wanaowanyonya au kuwatapeli waandishi. Ifahamike kuwa ili mrabaha uongezwe sharti bei ya kitabu pia iongezwe. Na athari ya kuongeza bei ya kitabu ni ghali kwani wasomaji wengi hawataweza kukinunua hivyo basi mauzo hupungua.

Mwandishi wa Kiswahili sharti aende na wakati na kuandikia maudhui yanayolenga jamii ya kisasa. Maudhui kama vile suala la ukimwi, mazingira, uana, nafasi ya elimu, utandawazi yanahitaji kupewa kipaumbele katika uandishi wa vitabu vya Kiswahili.

Aidha, vyuo vikuu vianzishe mafunzo ya uandishi kama taaluma katika idara za fasihi au Kiswahili au isimu na lugha. Haya yatakuwa maandalizi kabambe ya waandishi wa Kiswahili wa siku sijazo. Kozi zinazofundishwa katika vyuo vikuu kama vile Creative Writing (Utunzi wa Kisanii) au Editorial Methods (Mbinu za uhariri) ni fupi na sio toshelevu.

Waandishi wengi sana siku hizi wamejishughulisha na uandishi wa miswaada inayolenga mfumo wa vitabu vya shule hasa za msingi na za upili. Kumekuwa na ongezeko la fasihi ya watoto hasa vinavyowalenga wanafunzi wa shule za msingi. Kila mchapishaji anawaelekeza waandishi kutunga vitabu vya Kiswahili vinavyoweza kutumiwa kama vitabu vya ziada. Jambo hili linatokana na ukweli kuwa vitabu vya watoto kwa lugha ya Kiswahili vimekuwa vichache mno katika mfumo wa elimu nchini vikilinganishwa na vya lugha ya Kiingereza.

Madai kwamba vitabu vya Kiswahili havina soko hayana mashiko enzi hizi. Lugha ya Kiswahili inaendelea kupanuka kila uchao. Kwa mfano, kuna mpango wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda na bila shaka vitabu vya Kiswahili vitahitajika. Hili ni changamoto kwa waandishi wa Kiswahili, kujaribu kuona ni kwa namna gani wanaweza kufaidika kutokana na nafasi kama hii.

## 5. HITIMISHO

Makala hii imejadili suala la uandishi wa vitabu vya Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Kenya hasa masaibu yanayowakumba waandishi wa vitabu hivyo. Suala linalojitokeza ni kwamba waandishi wa vitabu vya Kiswahili hukumbana na visiki vingi katika harakati zao. Hata hivyo, vikwazo hivi visiwavunje moyo. Vikwazo hivi havina budi kutatuliwa na washika dau wote katika mfumo mzima wa elimu.

Kuna haja ya kushirikiana na kuaminiana kati ya mwandishi na mchapishaji. Aidha, serikali inapaswa kuanzisha chuo cha mafunzo za uandishi kwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma kama vile CHAKITA – Kenya. Pia, waandishi wa vitabu vya Kiswahili hawana budi kujibidiisha kufanya utafiti wa kina kabla ya kuandika vitabu vyao ili waweze kutoa vitabu bora vinavyotumiwa katika shule za msingi na za upili. Bila shaka taaluma ya uandishi wa vitabu hasa vya Kiswahili inatoa mchango mkubwa katika kufanikisha malengo ya elimu nchini Kenya.

## MAREJEO


Chachage, C. 1993.
*Kiungo Dhaifu kati ya Mwandishi na Jamii*. Katika **Fasihi, Uandishi na Uchapishaji**. Dar es Salaam: TUKI.

Habwe, J. 2002.
Uchapishaji wa Kazi za Isimu kwa Vyuo Vikuu nchini Kenya. Katika Kenneth Inyani (Mh), *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.

Kobia, J. 2004.
*Matatizo ya Uchapishaji wa Fasihi Simulizi Nchini Kenya*. Katika **Taifa Leo**, toleo la 19/10/2004.

Mallya, J. 1993.
Uandishi na Matatizo ya Uchapishaji Tanzania. Katika **Fasihi, Uandishi na Uchapishaji**. Dar es Salaam: TUKI.

Mbaabu, I. 1996.
*Language Policy in East Africa*. Nairobi: Educational Research and Publications.

Mbunda, F. 1983.
Misingi ya Uandishi wa Vitabu vya Kiada. Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili: Uandishi na Uchapishaji*. Dar es Salaam: TUKI.

Ministry of Education. 2005.
*Approved List of Primary School Textbooks and Other Instructional Materials*. Nairobi: MoEST.

Mung'ong'o, C. 1993.
Matatizo ya Waandishi Chipukizi. Katika **Fasihi, Uandishi na Uchapishaji**. Dar es Salaam: TUKI.
Robert, S. 1966.
*Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Nairobi: Nelson.

**About the author**: John M. Kobia is a Ph.D. candidate in the Department of Kiswahili and African Languages at Kenyatta University, Kenya. He holds B.Ed and M.Phil (Kiswahili) degrees from Moi University, Kenya. His publications and current research interests include gender studies, African oral literature, publishing, communication and African languages in education.